# JARIBIO LA MTIHANI
## DARASA LA SITA – 007
## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

___1___ kupata kiasi ___2___ fedha, Dama akatimiza azimio ___3___ kutoroka. Alienda kuishi ___4___ mji ___5___ uliokuwa kilomita hamsini ___6___ kwenye ule ___7___ kwanza, ___8___ akaanza ___9___ yake ya ___10___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Badala ya | B. Baada ya | C. Kati ya | D. Kando ya |
| 2. | A. hiyo ya | B. huo wa | C. hicho cha | D. hizo za |
| 3. | A. lake la | B. yake ya | C. wake wa | D. zake za |
| 4. | A. kwa | B. ndani | C. katika | D. katikati |
| 5. | A. mwingine | B. kwingine | C. nyingine | D. pengine |
| 6. | A. toka | B. kutoka | C. na | D. hadi |
| 7. | A. wa | B. ya | C. la | D. cha |
| 8. | A. labda | B. kama | C. kisha | D. vile |
| 9. | A. uhai | B. maisha | C. vituko | D. mwenendo |
| 10. | A. fahali | B. pahali | C. fahari | D. bahari |

Mahali hapo palikuwa pamejaa ___11___ wa watu. Wote walikuwa ___12___ makelele. "Mpige! Mpige! Mwue! Mwue! Lete tairi! Lete tairi!" Nilisongea kutaka kujua zaidi. Chini ___13___ ya mduara wa watu alikuwa barobaro ___14___ kama aliyekuwa ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. halaiki | B. umati | C. kundi | D. kaumu |
| 12. | A. wakapiga | B. wamepiga | C. walipiga | D. wakipiga |
| 13. | A. katikati | B. kati kati | C. kando ya | D. katika |
| 14. | A. aliyekunjuka | B. aliyekunja | C. aliyejikunja | D. aliyekunjika |
| 15. | A. usingizini | B. uzingizini | C. usingizi | D. uzingizi |



PRINTED BY KISTE PRINTERS

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa**

16. Jaza pengo kwa usahihi
Twende ________ mgonjwa tukamfariji.
A. kwenye B. kwa
C. kwao D. katika

17. Kamilisha tashbihi: Chungu kama
A. mkizi B. shubiri
C. jabali D. barafu

18. Kamilisha jina la makundi lifuatalo:
Mwanafunzi alibeba ______ la nguo
A. funda B. d-[illegible]
C. furushi D. korija

19. Ipi kati ya hizi ni sentensi sahihi?
A. Nilioga mikono.
B. Niliosha mikono.
C. Nilinawa mikono.
D. Nilisafisha mikono.

20. Twasema pakacha la matunda ilhali thurea ya·
A. mayai B. mwezi
C. maji D. nyota

21. Maana ya semi 'kupiga jeki' ni
A. kusaidia kimaisha
B. kuchekelea mtu
C. kutoroka mtu
D. kumsifu mtu

22. Hina kiganjani ni sawa na ________ machoni
A. kishaufu B. wanja
C. kipini D. kope

23. Kinengwe ina maana gani?
A. Mtoto wa punda
B. Mtoto wa papa
C. Mtoto wa bata
D. Mtoto wa nzige

24. Tegua itendawili:
Akopa na halipi ____________.
A. usingizi B. kifo
C. safari D. kazi

25. Chagua sentensi yenye 'ki' ya masharti
A. Kitoto cha jirani kimepotea
B. Alikuwa akilala nilipofika
C. Kila akimwona hufurahi
D. Akija mapema atampata

26. Iandike kwa nambari tarakimu hii:
Mia saba elfu na nane ____________
A. 700 0008 B. 70008
C. 7008 D. 700,008

27. Ipi orodha ya ala za kivita za kisasa?
A. Bunduki, risasi, guruneti, mzinga
B. Kombora, nyambizi, ngao, sime
C. Kombea, mshale, uta, mkuki
D. Kombora, kifaru, kombea, jambia

28. Chagua kundi la maneno ya vitenzi pekee:
A. Mweupe, mrembo, mdogo, laini
B. Vizuri, polepole, vibaya, haraka
C. Kaza, funga, aga, koroma
D. Kasha, mwizi, jangili, mbeni

29. Nini umoja wa:
Miti iliangukia kuta ndefu.
A. Mti uliangukia uta mrefu.
B. Mti uliangukia kuta refu.
C. Mti uliangukia ukuta refu.
D. Mti uliangukia ukuta mrefu.

30. Umbo la mpira wa kandanda laweza kuelezwa kuwa ni
A. mche B. duaradufu
C. mviringo D. tufe

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40***

Ni dhahiri shahiri kwamba mtu akikaa peke yake, au watu wakikaa katika makabila madogo bila kushirikiana na wengine, basi watakaa katika hali ile ile waliyo nayo, wala hawaendelei hata kidogo. Lakini mara wakianza kushirikiana na kupatana na wenzao

katika makabila na mataifa mengine, basi hapo wote hupata faida, maana watu hufundishwa mambo mapya wasiyoyajua na wote hufikiwa na nguvu za wenzao. Uzi mmoja hauna nguvu nyingi, lakini nyuzi nyingi zikisokotwa huwa kamba madhubuti inayoweza kumfunga ndovu asiweze kujijongeza wala kufurukuta kamwe.

Mapatano au ushirikiano ni jambo aula na adhimu zaidi katika maisha ya wanadamu. Zamani sana, watu hawakujua thamani ya kushirikiana kama wanavyofanya hivi sasa. Katika nchi hii yetu, wakati haujapita bado ambapo watu wengine wanakaa mbali katika makabila madogo au jamaa ndogo ndogo na jamii nyingine. Lakini kama taifa linataka kupiga hatua na kustawi kisiasa, kiuchumi na kijamii, ni sharti watu washirikiane - Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

31. Taifa lisilokuwa na umoja
   A. haliwezi kushinda vita
   B. haliwezi kustawi kiuchumi
   C. huwa na makabila madogo
   D. hukaa peke yake

32. Ni swala lipi lisiloambatana na ushirikiano kati ya makabila au mataifa?
   A. Maendeleo  B. Elimu mpya
   C. Kusaidiana  D. Kutumia nguvu

33. Nguvu za uzi mmoja katika taarifa ni mfano wa
   A. mtu mmoja mnyonge
   B. kabila moja lenye ushirikiano
   C. mataifa au nchi nyingi
   D. jamii au mataifa yaliyoungana

34. Mtu anaweza kujifunza kutokana na wengine kwa sababu
   A. akili nyingi huondoa maarifa
   B. ukijua huu, huu huujui
   C. asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
   D. akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

35. Taifa linaweza kuzorota kisiasa, kiuchumi na kijamii endapo
   A. halitapiga hatua kiuchumi
   B. halistawi katika kukuza uelewano
   C. halitatangamana na mataifa mengine
   D. halitatengana na mataifa mengine

36. Maneno 'jambo aula' maana yake ni
   A. jambo bora  B. jambo muhimu
   C. jambo zuri  D. jambo gumu

37. Kinyume cha neno kustawi ni
   A. kusinyaa  B. kulemaa
   C. kuzorota  D. kuduwaa

38. 'Kipiga hatua' ni sawa na
   A. kuendelea  B. kujulikana
   C. kusifika  D. kuheshimika

39. 'Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu' ni sawa na methali isemayo:
   A. Asiye na wake aeleke jiwe
   B. Kidole kimoja hakivunji chawa
   C. Akili ni nywele kila mtu ana zake
   D. Meno ya mbwa hayaumi

40. Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni
   A. Maendeleo katika jamii mbalimbali
   B. Umuhimu wa umoja na ushirikiano
   D. Mapatano miongoni mwa watu
   D. Ukabila ni adui

*Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50*

Siku moja, ubishi ulizuka baina ya viungo vya mwili. Viungo vya mwili vilikuwa vikilalamika kwa sababu vilikuwa vikifanya kazi zote lakini tumbo lilikuwa likila chakula chote bure bilashi. Basi vilifanya mkutano, mwishowe vikaafikiana vyote visusie kazi kwanza mpaka tumbo likubali kufanya kazi pamoja navyo.

Naam, kwa siku mbili tatu hivi, mikono ilikataa katakata kutwaa chakula. Kinywa kikagoma kukipokea kamwe, na meno hayakuwa na kazi abadan katan. Viungo hivyo vilizira mlo katu katu. Aha! baada ya radi huja mvua.

Haukupita muda, mwisho viungo vikajiona hata vyenyewe havikuwa katika hali njema. Mikono ilianza <u>kutaharuki</u> kwa shida na dhiki.

Kinywa chote kilikauka kama kisima cha jangwani. Miguu nayo ilinyong'olea na kulegalega kama utumbo wa samaki. Haikuweza kutegemeza sehemu nyinginezo. Kwa hivyo vikaona kwamba licha ya tumbo kuonekana halifanyi kazi, kumbe lilikuwa likishikilia kazi muhimu zaidi kwa masilahi ya mwili mzima. Fauka ya hayo, vyote vilikuwa havina budi kushirikiana kwa hali na mali katika kufanya kazi pamoja ama sivyo mwili wote utaangamia.

**41.** Kulingana na taarifa, ni wazi kuwa
A. viungo vingine vilidhania tumbo halifanyi kazi
B. viungo viyote viligoma kufanya kazi
C. mguu ulifanya kazi kubwa kuliko viungo vyote
D. tumbo hula bure halifanyi kazi

**42.** Ubishi ulizushwa na nani?
A. Viungo vyote vya mwili
B. Uzembe wa tumbo
C. Umuhimu wa tumbo
D. Baadhi ya viungo vya mwili

**43.** Ni maana ya neno kutaharuki kulingana na taarifa?
A. Kubabaika
B. Kuteseka
C. kuhamaki
D. kulegea

**44.** Kinywa kiligoma kufanya nini?
A. Kutia chakula mdomoni
B. Kupokea chakula
C. Kusaga chakula
D. Kuzungumza na tumbo

**45.** 'Viungo vikajiona havikuwa katika hali njema', kwa sababu
A. viligoma
B. viliasi tumbo
C. vilisusia kula
D. vilifanya mkutano

**46.** Kugoma kwa viungo
A. kuliathiri mwili mzima
B. kuliumiza tumbo zaidi
C. kulifanya tumbo liache uvivu
D. hakukuwa na madhara yoyote kwa tumbo

**47.** Viungo vilipokutana, viliamua kwamba
A. tumbo lifanye kazi
B. visusie kazi mpaka tumbo litakapofanya kazi
C. vifanye kazi hadi tumbo litakapofanya kazi
D. vifanye mgomo wa siku mbili tatu

**48.** Baada ya mikono kukataa kutwa chakula
A. meno yalilalamika
B. kinywa kilikauka
C. tumbo lilikasirika
D. miguu iliongea

**49.** Neno 'ulizuka' ni sawa na
A. ulianza
B. uligoma
C. ulishuka
D. ulifika

**50.** Habari hii inatufunza kwamba
A. Ibilishi wa mtu ni mtu
B. Jifya moja haliinjiki chungu
C. Wema hauozi
D. Adui mpende